# Ukurasa mmoja juu ya "uchochezi

**Mfumo wa kisheria:**

Kifungu cha 20, ibara ya 2 ya Mapatano ya Kimataifa juu ya Haki za Raia na za Kisiasa (ICCPR) kinasema kwamba "utetezi wowote wa chuki za kitaifa, kijamii au kidini ambao unajumuisha uchochezi wa ubaguzi, uadui au vurugu utakuwa kinyume cha sheria."

**Ufafanuzi:**

- Istilahi '**chuki**' na '**uadui**' zinarejelea hisia kali na zisizo na mantiki za dharau, uadui na chuki dhidi ya kikundi lengwa;
- Istilahi '**utetezi**' inapaswa kueleweka kama kuhitaji lengo la kuendeleza chuki kwa umma dhidi ya kikundi lengwa; na
- Istilahi "**uchochezi**" inarejelea kauli kuhusu vikundi vya kitaifa, kijamii au kidini, ambayo husababisha hatari kubwa ya kutokea kwa ubaguzi, uadui au vurugu dhidi ya watu wa vikundi hivyo.

**Zoezi la Kizingiti:**

Kifungu cha 20 cha ICCPR kinahitaji kizingiti cha juu kwa sababu kikomo cha uhuru wa kujieleza ni lazima kiwe jambo la kipekee. Mpango wa Utendaji wa Rabat (A/HRC/22/17/Add.4, kiambatisho) unapendekeza kwamba kila mojawapo ya sehemu sita za zoezi la vizingiti lifuatalo inahitaji kutimizwa ili kauli ihitimu kuwakosa la jinai:

(1) **Muktadha:** Muktadha ni muhimu katika kutathmini iwapo kauli fulani hasa inaweza kuchochea ubaguzi, uadui au vurugu dhidi ya kikundi lengwa, na inawezakutoa mwelekeo wa moja kwa moja kwa lengo na/au chanzo. Uchanganuzi wa muktadha unafaa kuweka tendo hilo la usemi ndani ya muktadha wa kijamii na kisiasa unaotamalaki kwa wakati huo ambapo usemi ulitolewa na kuenezwa.

(2) **Msemaji:** Nafasi au hadhi ya msemaji katika jamii inafaa kuzingatiwa, hasa msimamo wa mtu binafsi au shirika katika muktadha wa hadhira ambao walilengwa na matamshi hayo ya chuki;

(3) **Lengo:** Kifungu cha 20 cha ICCPR kinatazamia lengo. Uzembe na kutojali haziwezi kutosha kufanya tendo liwe hatia chini ya kifungu cha 20 cha ICCPR, jinsi kifungu hicho kinatolea "utetezi" na "uchochezi" badala ya usambazaji na uenezaji tu wa kitu. Kwa sababu hii, inahitaji uamilifu wa uhusiano wa pembe tatu kati ya mtendewa na mtendaji wa tendo la usemi pamoja na hadhira;

(4) **Yaliyomo na umbo:** Yaliyomo katika usemi huchangia mojawapo ya kitovu cha mashauriano ya korti na ni kipengele muhimu cha uchochezi. Uchanganuzi wa yaliyomo unaweza kujumuisha kiwango ambapo usemi huoulikuwa wa uchochea na moja kwa moja, sawa na umbo, mtindo, hali ya mabishano yaliyotolewa kwenye usemi huu au usawa uliopo kati ya mabishano yaliyotolewa;

(5) **Kiwango cha tendo la usemi**: Kiwango kinajumuisha vipengele kama ufikio wa tendo la usemi, hali yake ya umma, ukubwa wake na ukubwa wa hadhira yake. Vipengele vingine vya kuzingatia iwapo usemiulitolewa kwa umma, njia ya uenezwaji iliyotumika, kwa mfano karatasi moja au kutangazwa kwenye vyombo vikuu vya habari au kupitia Mtandao, idadi ya marudio, kiasi na kiwango cha mawasiliano hayo, iwapo hadhira ilikuwa na njia ya kutekeleza uchochezi huo, iwapo kauli hiyo (au kazi) imeenezwa katika mazingira yanayodhibitiwa au yanafikiwa kwa upana katika umma ya kawaida; na

(6) **Uwezekano, ukiwa ni pamoja na kukaribia kutokea kwake:** Uchochezi, kwa ufafanuzi, ni uhalifu unaoanza. Tendo linalotetewa kupitia usemi wa uchochezi si lazima litendwe kwa kauli iliyotajwa ili kuwa uhalifu. Hata hivyo, viwango vingine vya hatari ya madhara ni lazima vitambuliwe. Ina maana kwamba makorti yatalazimika kubaini kwamba kulikuwa na uwezekano wenye mantiki kwamba usemiungefanikiwa kuchochea tendo halisi dhidi ya kikundi lengwa, huku yakitambua kwamba chanzo kama hicho kinafaa kuwa moja kwa moja.

Mpango wa Rabat unadokeza kwa wasiwasi kwamba wahusika wa tukio, ambalo kwa kweli linaafiki vizingiti vya kifungu cha 20
cha ICCPR, hawafunguliwi mashtaka na kuadhibiwa. Wakati huo huo, wanachama wa walio wachache wanafunguliwa mashtaka halisi, yenye athari kali kwa wengine, kupitia kwa matumizi mabaya ya sheria zsizoelezwa wazi za nchi. Viongozi wa kisiasa na kidini wanastahili kuepuka kutumia uchochezi wowote wa chuki, lakini pia wana jukumu muhimu kukemea vikali na kwa wakati ufaao usemi wa chuki na wanafaa kuweka wazi kwamba vurugu haviwezi kukubaliwa kama jibu kwa uchochezi wa chuki (tazama pia 18 commitments on “Faith for Rights”).